

Mpango wa Watoto Wachanga wa North Carolina

**ukijua mapema, atakua vizuri**

# Mpango wa Mkopo wa Teknolojia Saidizi

## Maagizo ya Matunzo na Usafishaji

*Sehemu muhimu ya utunzaji wa kifaa cha teknolojia saidizi ni kusafisha baada ya kila matumizi au mara kwa mara. Matunzo na usafishaji unaofaa wa vifaa unawezesha familia yako kunufaika na kifaa hicho kabisa. Inasaidia pia kuhakikisha usalama wa mtoto wako.*

Ikiwa yapo, fuata maagizo ya mtengenezaji ya usafishaji wa kifaa. Vinginevyo:

- Tumia kitambaa cha kusafisha au sanitaiza kwenye tishu au sponji yenye unyevu kidogo kusafisha kifaa. Usinyunyuzie visafishaji moja kwa moja kwenye kifaa.
- Usitumie vitu vingi viowevu au visafishaji vyenye kamikali kali vinavyoweza kuharibu kifaa.
- Kausha kifaa ukitumia kitambaa baada ya kusafisha.



***Familia na watoto watafaidika na teknolojia saidizi katika maktaba ya mkopo ikiwa sote tutachukua muda wa kutunza na kusafisha ipasavyo.***

## Vidokezo Zaidi

- Ikiwa kifaa hakifanyi kazi vizuri au ukigundua matatizo yoyote (kwa mfano, vipande vilivyolegea, kukosekana kwa kamba) wasiliana na Mratibu wako wa Huduma za Suluhu za Mapema (EISC, Early Intervention Service Coordinator).
- Ikiwa kifaa kinatumia betri, kizime wakati hakitumiki.
- Hakikisha sehemu zote za kifaa, kama vile kamba na vifuniko vya betri vimeunganishwa, katika kipindi cha mkopo ili visipotee.




Maelezo ya Mawasiliano ya CDSA:

Jina la EISC:

Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya North Carolina www.ncdhhs.gov
Sekta ya Ustawi wa Watoto na Familia | Kitengo cha Suluhu za Mapema
N.C. DHHS ni mwajiri na mtoa huduma asiyebagua mtu yeyote. 12/11, 3/22, 1/23, 5/23

NC DEPARTMENT OF HEALTH AND HUMAN SERVICES
Division of Child and Family Well-Being
NC Infant-Toddler Program (NC ITP)

www.ncdhhs.gov/itp-beearly